# OFISI YA WAZIRI MKUU
# SERA BUNGE NA URATIBU

*JARIDA LA MTANDAONI* | *www.owm.go.tz* | *DODOMA* | *TOLEO LA JULAI 2022*




*KATIBU MKUU*
*OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE NA URATIBU*

*2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA*

*www.owm.go.tz*



# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 101 ZIMETENGWA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI.

Waziri wanchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amesema kupitia ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu pamoja na Taasisi zake iliidhinishwa na Bunge Zaidi ya shilingi Bilioni 101 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.61 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukilinganisha na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kwaajili ya utekelezaji wa Miradi ya Serikali.

Ameyasema hayo Julai 29, 2022 wakati akizungumza na waandishi wa habari ambapo amesema bajeti hii ya mwaka wa fedha 2022/2023 itaenda kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo kuratibu shughuli za Serikali, Menejimenti ya Maafa, kuchapisha na kuweka kumbukumbu za serikali (Mpiga chapa Mkuu wa Serikali) Miradi ya maendeleo, Mapambano dhidi ya Biashara na matumizi ya dawa za kulevya, Mapambano dhidi ya Ukimwi, pamoja na kukuza Demokrasia

pamoja ili kazi za serikali zielekezwe kwa ufanisi, kusimamia na kuchapisha nyaraka mbalimbali za serikali Bunge na Mahakama kwa kusimamia Nembo na Bendera ya Taifa , kutoa ubora na viwango vinavyotakiwa, kutengeneza mihuri mbalimbali, kuhifadhi nyaraka mbalimbali za serikali pamoja na kusanifu na kuhifadhi alama na siri katika machapisho ya nyaraka za Serikali".

"Uratibu wa Shughuli za Serikali unahusu kuweka wadau

Aidha Waziri Simbachawene amesema kwa mwaka wa fedha 2022/23 serikali imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 300 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na majengo ya Ofisi za Wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ,miundombinu ya Barabara,Umeme,Maji safi ,Maji taka na mifumo ya Tehama.

Hata hivyo Mhe. Simbachawene amesema Kwa upande wa kukuza Demokrasia kwa mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imeitengea Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Zaidi ya shilingi Bilioni 21 ili kuweza kutekeleza majukumu yake na ziaidi ya kiasi cha shilingi Bilioni 10 zimetengwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

"Serikali imekuwa ikifanya Jitihada mbalimbali zenye lengo la kukuza Demokrasia Nchini hivyo katika kuendeleza jitihada hizo Ofisi ya Waziri Mkuu itahakikisha inaandaa maeneo ya Uchaguzi na vituo vya kuandikia wapiga kura ,Mifumo ya Menejimenti,kuendesha vikao vya wadau wa vyama vya siasa,kutoa elimu ya mpiga kura pamoja na kukamilisha jingo la makao makuu ya Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa hapa Jijini Dodoma ambapo Zaidi ya kiasi cha shilingi Bilioni 20 zitatumia kukamilisha jingo hilo ambapo likikamiliaka litakuwa na nafasi ya vyama vyote vya siasa."

Waziri Simbachawene amemshukuru Rais samia kwa kukubali kuongeza Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika ofisi yake  ambayo itawezesha utekelezaji wa majukumu na kuleta tija na ufanisi katika kuratibu shuhguli za kiserikali.




## SERIKALI YAHIMIZA USHIRIKIANO KATIKA KUIMARISHA UTENDAJI WA KAZI SEKRETARIETI YA SADC

Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene ameishauri sekretarieti ya SADC kwa Kushiriiana katika kuimarisha  utendaji wa kazi wa Kituo cha udhibiti wa Maafa.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu katika Mkutano wa kamati ya Mawaziri wanaoshughulika na udhibiti wa maafa kwa Nchi wanachama wa SADC uliofanyika Lilongwe Nchini Malawi.

Katika kikao hicho waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu aliaambatana na Mkurugenzi wa Idara ya Maafa, Ofisi ya waziri Mkuu Meja Jenerali Michaeli .M. Mumanga aliyeongeoza ujumbe wa Tanzania katika Kikao hicho.



## *TANZANIA YAPIGA HATUA KUBWA KATIKA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA UKIMWI*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amesema vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kwa 50% kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2020.
" Maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020; na Maambukizi mapya kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (Mother to child transmission) yameshuka kutoka 18% mwaka 2010 hadi 7% mwaka 2020."
Hayo yamesemwa na waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene kwenye harambee ya uchangishaji wa fedha za kupanda mlima kilimanjaro ili kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI mwaka 2022.
Alieleza Matumizi ya dawa za kufubaza VVU (ARV) kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka 95% mwaka 2016 hadi 98% mwaka 2020;
Aidha maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020.
"Serikali, tayari imetenga fedha Bilioni 1.88 kwenye bajeti ya 2022/2023 ili iendelee kuchangia AIDS TRUST FUND alisema waziri"
Amefafanua serikali itaendelea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa afua zinazotekelezwa za Mwitikio wa VVU na UKIMWI zinaleta tija kwa makundi mbalimbali katika jamii.
Amesema ili kufikia malengo haya pamoja na mengine katika kuishinda vita hii dhidi ya VVU na UKIMWI, kunahitaji nguvu ya pamoja kati ya serikali na wadau wengine, hususan sekta binafsi ili kupata rasilimali fedha ya kutosha.
"Kili challenge inalenga kupunguza athari za kupungua kwa misaada ya wahisani na kuiwezesha Nchi kuimarisha uwezo wa ndani kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI"
Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Dkt. Leonard Maboko, amesema kutakuwa na wapanda baiskeli 28 kuuzunguka Mlima Kilimanjarao na wapandaji mlima kwa Mguu 24.
Kwa muda wa miaka 20 zoezi hili limekuwa likifanywa na kuchangia kiasi cha dola za kimarekani million 7 zimekusaywa na zimesaidia sana katika makabilia kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI mwaka.
Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Stephen Kagaigai, ameshukuru wadau wote walioshiriki kwa lango la kutafuta fedha za muitikio wa VVU na UKIMWI.
"Nimatumaini yangu kwamba ushirikiano huu utaendelea ili kufikia malengo ya sifuri tatu, kufikia mwaka 2030 ya kutokuwa na maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI. Kushuka kwa maambukizi ya UKIMWI ni matokeo ya pamoja ya Wadau wa sekta ya Umma na Binafsi"
Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania; Dkt. Leornad Maboko amesema fedha zinazopatikana katika harambee zitasaidia sana katika kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.
"Tumeunda kill Trust Fund, wajumbe wa bodi wanatoka upande (GGM) Geita Gold Mine na wengine wanatoka Tume ya Kudhibiti na Kupambana na UKIMWI, bodi imesaidia sana katika kuja na mikakati ya kufanya mara baada ya kukusanya Fedha"
Naye Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mgodi wa Geita Gold Mine Bwn. Simon Shayo, Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mgodi wa Geita (GGM); amesema tumekuwa tukikusanya fedha zinazosaidia maeneo mabalimbali, baadhi ya taasisi zimeasisiwa kutokana na uwepo wa mfuko huo ikiwemo kituo cha kulelea Watoto yatima Mkoani Geita.
"Kituo kilianza na Watoto 13 lakini sasa kina Watoto zaidi ya 170 ambao wanapata elimu wanapata huduma za afya kutokana na watu wanajitolea kuchangia kupitia Mfuko. Kundi la kwanza la Watoto walioingia kwenye kituo hicho wengi wao wako chuo kikuu"



## KATIBU MKUU DKT. JINGU AHIMIZA UFANISI UJENZI WA MJI WA SERIKALI

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. John Jingu azitaka Wizara zote kuhakikisha zinasimamia ufanisi na weledi katika ujenzi Awamu ya Pili wa majengo ya Ofisi zao katika Mji wa Serikali Mtumba.

Ameyasema hayo mapema alipokutana na Wakurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Wizara zote katika Ukumbi wa mikutano wa ofisi yake Jijini Dodoma kwa lengo la kujadili maendeleo ya ujenzi wa Ofisi za Wizara hizo zinzojengwa Mtumba Jijini Dodoma.

Dkt. Jingu alisema,kila wizara inajukumu la kuhakikisha majengo yanajengwa kwa viwango vinavyoendana na thamani ya fedha huku akiwataka kuendelea kufanya kazi kwa uzalendo kama ilivyoelekezwa.

"Viongozi wetu na wananchi kwa ujumla wana matarajio makubwa kuona mji wa Serikali unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa hatutarajii kuwa na delays,"alisema Dkt. Jingu

Aidha alizitaka kila Wizara kuendelea kuzingatia ubora katika kulifanikisha zoezi hilo huku wakiwasimamia wakandarasi na kuhakikisha kila vifaa vinavyonunuliwa vinakaguliwa na timu husika kabla ya matumizi.

Aliwasihii viongozi hao kuongeza rasilimali watu, vifaa na wataalamu ili kuweza kukamilisha ujenzi wa majengo hayo.

"kazi ya ujenzi izingatie viwango vilivyopo, katika hili tumeunda timu mbalimbali za kupitia na kukagua viwango ambapo tumewapa kazi BICO ya kufanya Quality assurance kuona mihimili ya majengo na mifumo mbalimbli ikiwemo ya maji, umeme na TEHAMA inakidhi vigezo hivyo naomba tuwape ushirikiano ili watimize kazi zao,"Alisisitiza

Hata hivyo Dkt. Jingu aliwasisitiza kuendelea kutoa taarifa za maendeleo ya ujenzi huo kila ifikapo tarehe 30 ya mwisho wa mwezi na kuwasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili kujua na kuwa na uhakikika wa kazi inavyoendelea.

Katika hatua nyingine aliwasihi kuendelea kutunza miti iliyopandwa katika maeneo ya ofisi zao kwa kuzingati umuhimu wake wa kuboresha mazingira na kuupamba mji huo.

"Kila Wizara ihakikishe inatunza miti iliyopandwa na kuzingatia mikataba ya upandaji wa miti katika Mji wa Serikali,"alisisitiza Dkt. Jingu



***MEJA JENERALI MUMANGA "MPANGO WA TAIFA WA KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAAFA KUPUNGUZA VIHATARISHI VYA MAAFA***

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Bw. Kaspar Mmuya amewashukuru wananchi waliohamia katika Kijiji cha Msomera awamu ya nne huku wakionesha furaha yao kwa kuanza maisha mapya ya katika kijiji hicho.

Ametoa pongezi hizo Julai 7, 2022 wakati wa zoezi la kuwapokea wananchi walihamia kwa hiari katika kijiji cha Msomera Wilayani Handeni kutoka katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha ikiwa ni kundi la nne toka zoezi hilo kuanza.

Alieleza kuwa katika awamu hiyo wamewasili jumla ya wananchi 188 wakiwa wenye furaha na kupongeza Serikali kwa uratibu mzuri wa zoezi hilo huku wakitarajia kuishi kwa amani na kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Aidha Mmuya alitumia fursa hiyo kuwaasa wananchi kutumia maeneo hayo kimkakati kwa kuanza kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizopo ikiwemo ufugaji wa kisasa utakao chagiza ongezeko la kipato kwa wakazi hao wapya.

"Kipekee namshukuru Rais wetu mpendwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha zoezi hili kufanyika kwa weledi mkubwa na hii inaonesha namna Serikali yenu inavyowajali, tunawaahidi tutaendelea kushirikiana na zitumieni fursa zilizopo Msomera,"alisema Mmuya

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mhe. Siriel Mchembe akizungumza wakati wa zoezi hilo alisema Wilaya yake imejipanga kuhakikisha inatoa ushirikiano usiku na mchana huku akiwahakikishia wananchi wote waliohamia katika eneo hilo watapata huduma zote muhimu ambapo amewasihi kubadili mitazamo na kujua kuwa wamekuwa wakazi rasmi wa Msomera.

Pia aliwataka kuhakikisha wanapeleka watoto shule kwa kuzingatia ni jambo muhimu na kuahidi kufanya sense ya kuhakikisha kila mtoto mwenye sifa ya kwenda shule anapelekwa ili kuwa na kizazi chenye elimu na kujikwamua kimaisha.

"Tujenge kizazi chetu hapa msomera chenye elimu, na mimi huu utakuwa ni wimbo wangu, hakikisheni mnapelekea watoto shule na nitafanya sense ya kuhakikisha kila mtoto anapata haki ya elimu,"alisema

Akitoa kauli ya ukiri wa kupokea wananchi na mifugo kwa awamu hiyo ya nne alisema mifugo yote itakayokuwa eneo hilo itunzwe na kuhakiksha inahudumiwa vyema ili ilete manufaa kwao na wakazi wengine wa Handeni hata nje ya hapo.

"Hadi leo ninakiri kumepokea jumla ya kaya 104 kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, idadi ya watu 690 ikiwemo watoto 102, ila kwa awamu hii ya nne nimepokea idadi ya watu 188 ambapo148 ni watu wazima na 40 ni watoto ,upande wa mifugo ninakiri kupokea jumla ya mifugo ikiwemo; ng'ombe 240, mbuzi 348, punda 22, kondoo 274 kwa ujumla ya idadi za mifugo toka awamu ya kwanza tumepokea jumla ya ng'omba 638, kondoo 516 na mbuzi 836 mifugo hii itunzwe na kuhakiksha inahudumiwa kwa usahihi,"alisisitiza Mhe Mchembe.

Naye Aliyekuwa Diwani ya Kakesio kutoka Ngorongoro Mhe. Johannes Tiamasi akitoa neno la shukran aliendelea kupongeza namna zoezi lilovyoearibiwa huku akiwasihi viongozi wenzake waliobaki Ngorongoro kuacha kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu maeneo ya Msomera ikiwemo dhana potofu juu ya zoezi zima la kuhamia katika eneo hilo.

"Msomera ni nzuri sana, ardhi ni nzuri niwatoe hofu waliobaki Ngorongoro kujiandikisha kwa kuzingatia nafasi ya kufanya hivyo bado ipo, hakika hili ni eneo la maziwa na asali hivyo tulikimbilie,"alisisitiza Tiamasi

Naye Mwenyekiti wa Msomera Bw. Martine Oleikayo Paraketi alieleza kwamba wataendelea kutoa ushirikiano kwa uongozi uliopo huku akiwaasa wananchi hao kuiona msomera yeye mazingira rafiki katika kila sekta ikiwemo uwepo wa miundombinu ya maji, mawasiliano, umeme, afya na elimu.

"Msomera kumenoga kwani kuna kila huduma muhimu tunayohitaji hivyo tujisikia vizuri kuwepo hapa na tuendelee kuishi kwa amani na upendo kwa kuzingatia nchi yetu ni kitovu cha amani tuijenge msomera yetu iwe ya mfano kwa wengine,"alisema Oleikayo



## MEJA JENERALI MUMANGA "MPANGO WA TAIFA WA KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAAFA KUPUNGUZA VIHATARISHI VYA MAAFA

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha Mpango wa Taifa ya Kujiandaa na kukabiliana na Maafa pamoja na Mkakati wa Mawasiliano wa Dharura unaolenga kupunguza vihatarishi vya maafa ili kuepusha madhara yatokanayo na maafa nchini.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Meja Jenerali Michael Mumanga wakati akiwasilisha hotuba kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu wakati wa ufunguzi wa Jukwaa la Taifa la Wadau wa Udhibiti wa maafa kwa ajili ya kuthibitisha Mpango huo lililofanyika Mount Meru hotel Mkoani Arusha lililokutanisha wadau kutoka Mashirika ya Umoja wa Mataifa na **Kimataifa,** Asasi za Kiraia na wawakilishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Meja Jenerali alieleza kuwa, kutokana na uwepo wa athari za maafa katika jamii Serikali kwa kushirikiana na wadau imeona ni muhimu kuwa na mipango na mikakati madhubuti yenye lengo la kujiandaa na kupunguza vihatarishi vya maafa kwa kadiri inavyowezekana ili kujenga jamii iliyo na ustahimilivu.

"Tunaamini jitihada za pamoja na wadau zitasaidia katika kukabili majanga nchini kwani kumekuwa na matukio ya majanga ambayo yamekuwa yakisababisha maafa na kuathiri mfumo wa kawaida wa maisha katika jamii kupelekea matokeo hasi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kutokana na kupotea kwa mafanikio yaliyopatikana kwa muda mrefu na hivyo kuzorotesha hatua za maendeleo

Aidha alisema majanga yapo mengi ya asili na yatokanayo na shughuli za kibinadamu hivyo ipo haja ya kila mmoja wetu kwa kushirikiana na wadau kufanya kazi kwa ufanisi kuhakikisha tunasaidia jitihada hizi za kukabiliana na maafa.

"Maafa yapo kila sehemu yanatofautiana kwa vyanzo vyake, hivyo mpango huu umekuwepo tangu 2012 ni kweli kwamba ipo haja ya kuuhuisha kwa kuzingatia muda na matukio yanabadilika, hivyo kuhuishwa kwa mpango huu kutaendana na hali halisi ya sasa ya kukabiliana na maafa nchini,"alisisitiza.

Kwa upande wake Mkuu wa uendeshaji UNDP Bw. Bwana Jeremiah Mallongo akiwaslilisha hotuba kwa niaba ya Mratibu mkazi wa shirika hilo alisema jukwaa hilo limewakutanisha kwa siku tatu na kueleza litasaidia kuhuisha mpango ili kuwa na uhalisia katika kukabili maafa, hivyo lengo ni kuendelea kupunguza vihatarishi vya maafa na athari zake.

"UNDP tunafuraha kuratibu jukwaa hili kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha tunaendelea kuweka mikakati ya kupunguza athari za majanga nchini kwani majanga yatakuwepo kutokana na sababu mbalimbali ila lengo kuu ni kuweza kuyakabilia na kupunguza athari zake,"alisema Mallongo

Naye Naibu Kamishna Operesheni kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Bw.Charo Mangale amewasihi wananchi kuendelea kutoa taarifa za majanga mapema kunusuru athari zitokanazo na janga hilo huku akieleza ofisi yake imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna bora ya kukinga na maafa pindi yanapotokea.

"Ofisi yetu imeendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya majanga mbalimbali, nitoe rai kwa wananchi kabla ya janga halijatokea pokea elimu ambayo imekuwa ikitolewa na Jeshi la zimamoto kupitia askari wetu wanaopita milango kwa milango ili janga linapokea unakuwa na mbinu za kukabili pia taarifa zitolewe mapema kupitia namba 114 ni namba ya dharura na ni bure, tutakufikia na kukupoa huduma," alisema Mangale



## *HALMASHAURI YA MERU YAPATA ELIMU YA KUKABILIANA NA MAAFA*

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa, Luteni Kanali Selestine Masalamado amesema elimu ya usimamizi wa Maafa itaendelea kutolewa kwa wananchi kwa maeneo yanaoathirika kwa matukio ya tofauti tofauti ya maafa.

"Tunatoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wanamna ya kukabiliana na maafa, kwa kueleza dhana ya maafa, kueleza maana ya majanga ikiwa pamoja na kuangalia mzingo wa maafa kwa ujumla"

Hayo yamesemwa na Luteni Kanali Selestine Masalamado Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu kwa kushirikiana na shirika la kimataifa la uhamiaji (IOM) katika kikao cha mafunzo ya Udhibiti wa Maafa kwa jamii yaliyofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Meru na kuhusisha wananchi wa kata ya Mbuguni na Shambaray Bruka.

"Washiriki wameelewa mfumo mzima wa Kudhibiti Maafa kwa kuanzia ngazi ya taifa hadi kufikia ngazi ya Kijiji, alisema Luteni Kanali"

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya ameshukuru Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu kwa kufanya mafunzo hayo Halmashauri ya wilaya ya Meru.

"Tunashukuru kwa kutuongezea wataalamu wa maafa kupitia mafunzo yaliyoyotolewa ili kutusaidia namna ya kukabiliana na Maafa."

Mwl. Makwinya amefanunua kata ya Shambaray Bruka na Mbuguni yamekuwa yakiathirika na mafuriko na ukame,

Ametoa wito kwa washiriki kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza maarifa kwa kusaidia maeneo mengine yanayoyoathirika na maafa.

Naye Mshiriki Fanael Kaaya Mshiriki kutoka kata ya Mbuguni amesema mafunzo ya kukabiliana na maafa waliyopata imesaidia kuchukua tahadhari ya kujikinga na maafa kabla hajatokea ikiwemo kutengeneza matuta ya kuzuia maji kwenye maeneo yanayoathirika na mafuriko na pamoja kufukua mifereji iliyoziba pamoja na mito ili mafuriko ya maji yanapokuja yaweze kupita.

**MATUKIO KATIKA PICHA WAKATI WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE NA URATIBU MHE. GEORGE SIMBACHAWENE ALIPOSHIRIKI MAADHIMISHO YA KUMBUKUMBU YA SIKU YA MASHUJAA JIJINI DODOMA**
















*KATIBU MKUU*
*Ofisi ya Waziri Mkuu*
*2 Mtaa wa Relini, S. L.P 980*
*40480 Dodoma,*
*Barua pepe;ps@pmo.go.tz, Simu;+255262322480*
*Fax:+255262324534, Tovuti:wwww.pmo.go.tz*